# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**
**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0787665009**
**Makamu Mkuu wa Shule 0616061485**
**Matron/Patron 0624835226**
**Shule ya Sekondari RANGWI**
**S.L.P. 238 LUSHOTO**
**Tarehe 26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RANGWI HALMASHAURI YA LUSHOTO MKOA TANGA MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024** na atasoma tahasusi ya ………… Shule ya Sekondari **RANGWI** ipo umbali wa Kilometa **50** Kaskazini mwa Mji wa **LUSHOTO** Usafiri wa basi kutoka **LUSHOTO** mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **LUSHOTO** Nauli ni Shilingi **8000/=** kwa basi. Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Suruali mbili (02) za rangi ya Maroon (Damu ya mzee) kwa Wavulana zenye marinda mawili ya mbele na turn up kwa chini na upana usiopungua 15 inch
ii. Mashati mawili (02) meupe ya mikono mirefu (Tomato).
iii. Sare ya Michezo ni
   a) Tracksuits ya blue yenye nembo ya shule pea moja, Tsh 25,000/= yenye michirizi myeupe mikononi na

miguuni (Vinapatikana duka la shule kwa mzazi atakayependa kununua shuleni)

b) Raba Nyeupe pea moja.

c) Tshirt ya michezo moja (01) ya blue yenye nembo ya shule Tsh 15,000/= (Inapatikana kwenye duka la shule kwa mzazi anayependa kununua shuleni)

iv. Viatu vya shule ni vyeusi pea mbili vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili (02) nyeusi za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Masweta mawili (02) kila moja ni Tsh 17,000/= rangi ya Maroon (Damu ya mzee) yenye nembo ya shule vitapatikana kwenye duka la shule kwa mzazi atakayependa kununua shuleni.

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*);
Suruali mbili (02) zenye rangi nyeusi isiwe ya kubana.

ix. Tai moja rangi ya maroon yenye michirizi nyeupe

x. Tisheti (T-shirt) mbili (02) rangi ya Orange yenye nembo ya shule ”Form Six” zinazopatikana katika duka la shule.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari kumi (10) Quire 3

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*English Language, History, Kiswahili, Geography, General Studies, Literature in English na Fasihi ya Kiswahili*)

iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanasoma Geography

v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni lenye vipimo vya futi 2½ kwa 6

vi. Mashuka ya bluu bahari Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1 na chandarua 1 rangi ya blue bahari.

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

x. Kwanja 1, jembe 1, squizer (mopa) 1, toilet sink brush 1 na hardbroom 1.

xi. Uje na **Bima ya Afya** kama huna unapaswa kuwa na fedha ya akiba itakayokusaidia katika matibabu.

xii. Sanduku imara la bati (tranker) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako.

xiii. Fika na **results slip** ya kidato cha nne inayoonesha matokeo yako ya kidato cha nne.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB; Fedha zote za michango mbalimbali ya shule zilipwe kwenye akaunti ya shule, isipokuwa fedha za Tshirt, Sweta na Tracksuit**
**Akaunti namba 41601100008 benki NMB**
**Jina la Akaunti RANGWI SECONDARY SCHOOL**
**Mwanafunzi aje na Bank Pay Slip (BPS) baada ya malipo kufanyika.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
**xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;**
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi

iii. Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iv. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

v. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule** **<u>REMINISERI BARIKI MARIKI</u>**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………………..**

THE HEADMASTER RANGWI SECONDARY SCHOOL P.O BOX 238 LUSHOTO

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule**:** **0787665009**
- Makamu Mkuu wa Shule **0616061485**
- Mwandamizi Taaluma **0621431660**
- Mwandamizi Malezi **0624835226**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PMO- REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

RANGWISECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 238,
**LUSHOTO.**
**24/04/2024.**

Ref. No. **RASS/J/F.V/VoI.1/2024.**
To the Medical Officer
…………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………..

**RE: STUDENT`S MEDICAL EXAMINATION FORM**

Please examine the pupil …………………………………………………………………………………….. in respect of these areas and any other area (s) deemed fit please. Delete whichever not applies.

Does the pupil have problems in connection with

a) Sight. Yes/ No. If yes, state
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

b) Hearing. Yes/No. If yes, state
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

c) Any other problem
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………..

Name…………………………….....Signature………………………Date ……………..
Official title ……………………………….
Official stump………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS: TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**

**SHULE YA SEKONDARI RANGWI**

PICHA NA NAMBA ZA SIMU ZA WAZAZI/WALEZI N A NDUGU WATAKAOWASILIANA NA MWANAFUNZI AU KUFIKA KUMUONA AWAPO SHULENI

1.

JINA:
……………………………………………
…………………………………………..

UHUSIANO NA MWANAFUNZI:
………………………………
NAMBA YA SIMU:
…………………………………………

2.

JINA:
………………………………………
……………………………………….

UHUSIANO NA MWANAFUNZI:
………………………………
NAMBA YA SIMU:
……………………………………

3.

JINA:
………………………………………………

UHUSIANO NA MWANAFUNZI:…………..
NAMBA YA SIMU:…………………….

4.

JINA:
……………………………………

UHUSIANO NA MWANAFU ……………………
NAMBA YA SIMU …………